



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA



HALMASHAURI YA WILAYA YA URAMBO

(Barua zote zitumwe kwa Mkurugenzi Mtendaji Wilaya)

Simu Na 2988305/2988324

Nukushi Na. 2988258

Barua pepe: ded@uramboc.go.tz

Tovuti: www.urambodc.go.tz

Unapojibu tafadhali taja:

Mkurugenzi Mtendaji (W)

30 Br. ya Boma Stendi,

S.L.P 170.

45582 Urambo-Tabora.

Kumb.Na.UDC/W.I/254/VOL.I/56

Tarehe: 01/06/2023

TANGAZO LA NAFASI YA KAZI YA MUDA/MKATABA

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Urambo anawatangazia Watanzania wote wenye sifa na nia ya kufanya kazi katika Halmashauri ya Wilaya ya Urambo kuomba nafasi ya kazi ya muda / Mkataba wa Miezi Mitatu kama ilivyotajwa hapo juu.

1.0 MTEKNOLOJIA DARAJA LA II (Nafasi 01)

1.1 SIFA ZA MWOMBAJI

Mwombaji anatakiwa awe na Elimu ya kidato cha nne (IV) au sita (VI), aliyehitimu mafunzo ya Stashahada ya Uteknolojia katika moja ya fani ya Radiografa – Radiolojia kutoka chuo kinachotambuliwa na Serikali na ambae amesajiliwa na Baraza la Wataalamu wa Radiolojia na Picha Tanzania (MRIPC)

1.2 MSHAHARA

Ngazi ya Mshahara ni TGHS B₁.

1.3 KAZI/MAJUKUMU YA MTEKNOLOJIA DARAJA LA II


- i. Kuwapima wagonjwa wanaoelekezwa kwenye eneo lake la kazi.
- ii. Kutunza mitambo na vifaa vya Radiolojia / X- Ray katika eneo lake la kazi.
- iii. Kutoa ushauri kuhusu masuala ya kazi za Radiolojia na Mionzi.
- iv. Kutoa mafunzo ya awali kwa watumishi wanaopangiwa kazi katika eneo lake la kazi.
- v. Kuandaa vifaa vya tiba/uchunguzi na kusimamia utakasaji vifaa katika eneo lake la kazi (sterilization).
- vi. Kutunza picha za wagonjwa hadi majibu yanapowafikia madaktari waliowatuma wagonjwa.
- vii. Kufanya kazi nyingine atakazopangiwa na mwajiri wake.

MAELEKEZO YA JUMLA KWA WAOMBAJI

- i. Waombaji wote wawe ni raia wa Tanzania wenye umri kati ya miaka 18 na usiozidi 45
- ii. Maombi yaambatanishwe na taarifa ya maelezo binafsi (Curriculum Vitae) ya muombaji ikionesha Wadhamini watatu na taarifa zao sahihi namba za simu za muombaji na wadhamini, cheti cha taaluma, cheti cha kidato cha nne, cheti cha kuzaliwa, na picha mbili passport size (ziandikwe majina kwa nyuma).
- iii. Testimonial na provisional statement of results hati ya matokeo ya kidato cha nne na sita havitapokelewa.
- iv. Waombaji waliostaafu/kustaafishwa au kuacha kazi katika Utumishi wa Umma hawarusiwi kuomba isipokuwa kwa kibali cha Katibu Mkuu Kiongozi.
- v. Muombaji atakaye wasilisha taarifa za kughushi atachukuliwa hatua za kisheria kwa mujibu wa taratibu
- vi. Barua zote ziandikwe kwa mkono kwa lugha ya Kiswahili au kiingereza.
- vii. Mwombaji awe hajawahi kupatikana na kosa la jinai au kufungwa jela.
- viii. Waombaji walisoma nje ya nchi waambatanishe cheti cha ulinganifu (Equivalent Certificate) kutoka baraza la Mitihani la Tanzania.
- ix. Watakoachaguliwa kufanya usaili watajulishwa tarehe ya usaili kwa njia ya simu pia kupitia tovuti ya Halmashauri www.urambodc.go.tz pamoja na mbao za matangazo.
- x. Mwisho wa kupokea maombi ni tarehe **14/06/2023** saa tisa na nusu (9:30) mchana.

Maombi yote yatumwe kwa njia ya Posta kwa anwani ifuatayo:-

Mkurugenzi Mtendaji Wilaya
30 Br. ya Boma Stendi,
S.L.P 170.
45582 Urambo-Tabora.



Baraka M. Zikatimu
Mkurugenzi Mtendaji
Halmashauri ya Wilaya
Urambo

MKURUGENZI MTENDAJI
HALMASHAURI YA WILAYA